**S.M.Z**

**BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR**

**MTIHANI WA DARASA LA NNE**

**123** **SAYANSI**

**Time: 1:30 Hours.** **SOLUTIONS** **Year: 2020**

---

**MAELEKEZO KWA WATAHINIWA**

**1. Mtihani huu una sehemu MBILI (2) A na B.**

**2. Jibu maswali YOTE katika sehemu A na B.**

**3. Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.**

**4. Majibu YOTE yaandikwe katika nafasi zilizowekwa.**

**5. Tumia kalamu ya buluu au nyeusi kwa kuandikia na penseli kwa kuchorea tu.**

**6. Simu ya mkononi na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi ndani ya chumba cha mtihani.**

maktaba.tetea.org
TETEA



Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

***Prepared by Maria Marco for TETEA***

SEHEMU A: (ALAMA 40)

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.

1. Chagua jawabu sahihi kisha andika herufi yake kwenye jadweli hapo chini ya maswali.

   i. Mswaki kazi yake ni

   A. Kunawia uso

   B. Kufulia nguo

   C. Kusafishia meno

   D. Kusafishia choo

Jibu sahihi ni C. Kusafishia meno. Mswaki hutumika kuondoa uchafu na vijidudu kwenye meno ili kuzuia kuoza kwa meno na magonjwa ya kinywa.

ii. Vyanzo vya maji ni

A. Mvua, mto na kisima

B. Chemchem, mfereji na kisima

C. Bahari, mto na tenki

D. Kisima, shimo na chemchem

Jibu sahihi ni A. Mvua, mto na kisima. Hivi ni vyanzo halisi vya asili vinavyotoa maji yanayotumika na binadamu.

iii. Miongoni mwa aina za misitu ni

A. Misitu ya moja kwa moja

B. Misitu mizuri

C. Misitu ya asili

D. Misitu inayovutia


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

***Prepared by Maria Marco for TETEA***

Jibu sahihi ni C. Misitu ya asili. Misitu ya asili hukua yenyewe bila kupandwa na binadamu.

iv. Moja kati ya vyanzo vya hewa ni

A. Maji

B. Feni

C. Dirisha

D. Kiyoyozi

Jibu sahihi ni C. Dirisha. Dirisha huruhusu hewa kuingia na kutoka ndani ya nyumba.

v. Mlo wenye virutubisho vyote vya chakula huitwa

A. Vyakula mchanganyiko

B. Chakula bora

C. Matunda na mboga mboga

D. Mlo kamili

Jibu sahihi ni D. Mlo kamili. Mlo kamili una virutubisho vyote muhimu kwa mwili.

2. Andika kweli au sikweli katika maelezo yafuatayo kwenye jadweli hapo chini.

i. Tumia gongo bichi kumnasua aliyenasa katika umeme.

Jibu ni Kweli. Gongo bichi halipitishi umeme hivyo ni salama katika hali hiyo.

ii. Mimea isiyotoa maua haina tunda halisi.

Jibu ni Kweli. Mimea isiyotoa maua haitengenezi tunda halisi.

iii. Wanyama wasiofugwa huhitaji uangalizi wa binadamu.

Jibu ni Sikweli. Wanyama wasiofugwa hujitegemea porini bila uangalizi wa binadamu.

iv. Udongo ni tabaka la juu la ardhi.

Jibu ni Kweli. Udongo hufunika sehemu ya juu ya ardhi.

v. Utupaji taka kwenye vyanzo vya maji hutupatia maji safi na salama.

Jibu ni Sikweli. Utupaji taka huchafua maji na kuyafanya yasiwe salama.

3. Oanisha maelezo ya kifungu A kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kifungu B. Andika herufi tu kwenye jadweli hapo chini.

KIFUNGU A

i. Majani yake huwa membamba na yenye ncha

ii. Hutengeneza chakula kwa msaada wa jua, hewa na maji

iii. Faida za misitu

iv. Mimea inayohifadhi chakula kwenye majani

v. Hutoa matunda na mbegu

KIFUNGU B

A. Muembe na mchungwa

B. Mboga

C. Kitunguu maji na kabichi

D. Husababisha mvua

E. Mchaichai na mua

F. Majimbi

G. Mimea

H. Mchaichai na muhogo

i. Jibu sahihi ni E. Mchaichai na mua. Mimea hii ina majani membamba yenye ncha.

ii. Jibu sahihi ni G. Mimea. Mimea hutengeneza chakula kwa msaada wa jua, hewa na maji.

iii. Jibu sahihi ni D. Husababisha mvua. Misitu huchangia upatikanaji wa mvua.

iv. Jibu sahihi ni C. Kitunguu maji na kabichi. Mimea hii huhifadhi chakula kwenye majani.

v. Jibu sahihi ni A. Muembe na mchungwa. Mimea hii hutoa matunda yenye mbegu.

4. Jaza nafasi zilizoachwa wazi. Tumia maneno yaliyomo kwenye kisanduku hapo chini ya maswali.
   (pamba, VVU, kiu, mpini, machafu, UUV, kitambaa, mshipi)

i. Kinakuwemo kwenye kisanduku cha huduma ya kwanza na hutumika kusafishia kidonda ______________________.

Jibu ni pamba. Pamba hutumika kusafishia na kufunika vidonda.

ii. Tunapohisi ____________________________ tunakunywa maji.

Jibu ni kiu. Kiu ni hali ya mwili kuhitaji maji.

iii. Ufupisho wa virusi vya Ukimwi ni _________________________.

Jibu ni VVU. VVU ni Virusi vya Ukimwi.

iv. Gongo refu linalochongwa vizuri na kuingizwa kwenye jembe ni ____________________________.

Jibu ni mpini. Mpini hushikilia chombo kama jembe.

v. Mtaro ni msingi ambao hutumika kupitisha maji ______________________.

Jibu ni machafu. Mitaro hupitisha maji machafu au ya mvua.

SEHEMU B: (ALAMA 60)

Jibu maswali YOTE kwenye sehemu hii.

5. a) Andika madini mawili (2) yanayopatikana kwenye udongo.
   i. Chuma. Chuma hupatikana ardhini na hutumika kutengeneza vifaa mbalimbali.
   ii. Shaba. Shaba ni madini yanayotumika sana katika umeme.

   b) Bainisha vitu viwili (2) vinavyotengenezwa kwa njia ya ufinyanzi.
   i. Chungu. Hutumika kuhifadhi au kupikia chakula.
   ii. Sufuria ya udongo. Hutumika kupikia vyakula.

   c) Taja viumbe viwili (2) vinavyoishi kwenye udongo.
   i. Minyoo. Husaidia kurutubisha udongo.
   ii. Sisimiz. Huishi na kuchimba mashimo ardhini.

6. a) Nini maana ya kipima joto?

   Kipima joto ni kifaa kinachotumika kupima kiwango cha joto cha kitu, mazingira au mwili wa binadamu.

   b) i. Kuna aina ngapi za kipima joto?

   Kuna aina mbili za kipima joto.

   ii. Zitaje

   Kipima joto cha kitabibu na kipima joto cha maabara.

c) Bainisha njia kuu tatu (3) za kusafiri kwa joto.

i. Upitishaji. Joto husafiri kupitia vitu vigumu kama metali.

ii. Mzunguko. Joto husafiri kupitia vimiminika na gesi.

iii. Mionzi. Joto husafiri bila kuhitaji kiungo kama kutoka jua.

7. a) Nini maana ya kipigi?

Kipigi ni mwanga wa rangi mbalimbali unaoonekana angani baada ya mvua kunyesha na jua kuangaza.

b) Kipigi kinafanyika vipi?

Kipigi hutokea pale mwanga wa jua unapopita kwenye matone ya maji ya mvua na kuvunjika kuwa rangi tofauti.

c) Taja rangi zote zilizomo kwenye kipigi.

Nyekundu, machungwa, njano, kijani, bluu, indigo na zambarau.

8. a) Nini maana ya mwangwi?

Mwangwi ni kurudi kwa sauti baada ya kugonga kitu kigumu kama ukuta au mlima.

b) Orodhesha vitu vinne (4) vinavyosababisha kufanyika kwa mwangwi.

i. Ukuta.

ii. Mlima.

iii. Mwamba.

iv. Jengo refu.

c) Andika sehemu mbili (2) ambazo mwangwi hutumika.

i. Mapangoni.

ii. Kwenye kumbi kubwa.

9. a) Nini maana ya uvunaji wa maji?

Uvunaji wa maji ni njia ya kukusanya na kuhifadhi maji ya mvua kwa matumizi ya baadaye.

b) Kamilisha jadweli lifuatalo kwa kuchagua maneno sahihi yaliyomo ndani ya mabano.
(uzi, maji, maziwa, mbao, upepo)

VITU YABISI: uzi, mbao

VIMIMINIKA: maji, maziwa

HEWA: upepo

c) Taja sifa tatu (3) za maji safi na salama.

i. Hayana rangi.

ii. Hayana harufu.

iii. Hayana ladha.

10. Picha zifuatazo zinaonesha vitendo gani?

i. kusafisha/kudeki choo

ii. Ususi

iii. Kufagia

iv. Kupika chakula.

v. Kufuga